

Wakati wapangaji wanaweka sainsi kwa hati ya kukodisha wanakubali masharti na hali katika hati.

Kama mpangaji akivunja sharti ya mkataba wa kupangisha anaweza kufukuzwa upangaji.

Kufukuza upangaji maana yake ni unahitaji kuondoka miliki ya kukodisha.

Ajenti au kabaila awe na sababu nzuri chini ya sheria kufukuza upangaji au kubatilisha mkataba wako wa kupangisha.

Lazima ajenti au kabaila akupe ilani ya mwisho wa upangaji ya maandishi kuelezea sababu na wakati uhama.

Kwa mfano, waweza kupokea ilani ya mwisho wa upangaji ukichelewa kulipa kodi kwa siku 14.

### **Utafanyaje ukipokea ilani ya mwisho wa upangaji?**

Kama ukipokea ilani ya mwisho wa upangaji, usiepuke, pata msaada mara moja.

Wasiliana na Tenants Advice and Advocacy Services or (TAAS) (Huduma za Ushauri na Utetesi wa Wapangaji) kupata ushauri.

### **Nini itakachotokea kama sihami miliki?**

Kabaila anaweza kuomba kwa Tribunal kumaliza upangaji wako usipohama baada ya notisi ya siku 14.

Kama hiyo inatokea Tribunal atakutuma barua na tarehe na anwani ya hukumu.

Uhudhurie hukumu ya Tribunal ili ueleze upande wako wa matokeo.

Ambia Tribunal ukihataji mkalimani. Mkalimani ni bila malipo.

Tribunal iatamua kama upangaji wako utamalizika

### **Je, unaweza ku bila notisi?**

Ndiyo, katika hali ifuatayo:

- matumizi nje ya sheria ya miliki
- kama ukisababisha madhara makali kwa milki au kwa milki ya jirani

- au kama ukiumiza au kutisha kabaila, ajenti, wafanyakazi au majirani

Kama ukifukuzwa upangaji waweza kuandikiwa kwenye orodha ya upangaji.

Hii inaweza kuleta ugumu kwa wewe kupanga miliki baadaye.

### **Orodha ya upangaji ni nini?**

Orodha ya upangaji ni orodha ambayo maajenti wanaweka maelezo kuhusu wapangaji wanaokuwa na matatizo na upangaji wako.

Inajulikana pia kama orodha ya watu watakaoadhibiwa au orodha ya wapangaji wabaya.

Waweza kuandikiwa kwenye orodha baada ya upangaji wako umemaliza na kama ulikuwa na deni ya pesa zaidi kuliko dhamana.

Kufahamu kama umeandikiwa kwenye orodha ya upangaji enda kwa sehemu ya mpangaji ya orodha hiyo ya upangaji

Tenancy Information Centre Australasia (TICA)  
[www.tica.com.au](http://www.tica.com.au)

National Database (NTD)  
[www.ntd.net.au](http://www.ntd.net.au)

Trading Reference Australia (TRA)  
[www.tradingreference.com](http://www.tradingreference.com)

Ada inaweza kutozwa kutumia maelezo hayo.

Tribunal inasimamisha mabishano kuhusu ilani ya mwisho wa upangaji, kufukuza upangaji na orodha ya upangaji.

Kufahamu kuhusu kazi ya Tribunal angalia DVD yao kwa YouTube au tembelea tovuti yao.

Kupata maelezo zaidi kuhusu haki na majukumu ya wapangaji, tembelea tovuti ya Fair Trading kwa [www.fairtrading.nsw.gov.au](http://www.fairtrading.nsw.gov.au) au piga simu namba ya 13 32 20.

Kama ukihataji msaada wa lugha pigia simu 13 14 50.